

IDS

UNIVERSITY OF NAIROBI  
L.D.S. LIBRARY



**Sekta Isiyo  
ya Kibashara  
Nchini Kenya**

*Tunayojua na tusiyojua*

Toleo pendelevu

Karuti Kanyinga na Winnie Mitullah

Kimetafsiriwa na Kithaka wa Mberia



THE INSTITUTE FOR DEVELOPMENT STUDIES  
UNIVERSITY OF NAIROBI

A K D N

AGA KHAN DEVELOPMENT NETWORK

## Dibaji

Taasisi ya Masomo ya Maendeleo (IDS), Chuo Kikuu cha Nairobi, imekuwa ikishughulikia utafiti wa kuonyesha ukubwa, muundo na upeo wa sekta isiyo ya kibiashara nchini Kenya.

Utafiti huu ulifanywa kama sehemu ya Mradi wa Linganishi wa Mashirika wa Centre for Civil Society Studies (CCSS) katika Chuo Kikuu cha Johns Hopkins. Kazi hii ilitekelezwa kwa ufadhili kutoka Afisi ya Afrika Mashariki ya Ford Foundation pamoja na Aga Khan Foundation.

Ingawa matokeo ya utafiti wa IDS kuhusu sekta isiyo ya kibiashara tayari yameenezwa kuititia mikutano na machapisho kadhaa kwa msaada wa Aga Khan Foudation, IDS imeonelea kwamba ni jambo zuri kuchapisha kitabu ili kufahamisha umma, waundaji sera, wafadhili, wale wanaoshughulikia maendeleo na washika dau wengine kuhusu muundo, upeo, ukubwa na ugharamiaji wa sekta hii nchini Kenya. IDS inatumaini kwamba kitabu hiki kitatumika kama marejeleo muhimu kwa masomo ya sekta hii nchini Kenya. Kwa hivyo, matokeo haya yanatupatia hatua ya kwanza muhimu ya ufahamu kamili wa sekta hii nchini Kenya, na zaidi ya hayo, kuunda msingi mzuri kwa watu wengine ambao wangependa kutafiti sekta hii.

Nchini Kenya, miongo minne iliyopita imeshuhudia mabadiliko muhimu katika masuala ya maendeleo. Serikali ndiyo iliyochukua jukumu kubwa kuhusu maendeleo miaka ya 1960 na 1970. Mashirika

ya umma ndiyo yalichangia pakubwa katika kuleta maendeleo ya kijamii. Jambo hili lilibadilika kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1980 kuambatana na kudidimia kwa uwezo wa serikali wa kuwa mhimili wa maendeleo ya kijamii. Kuanzishwa kwa Mradi ya Marekebisho ya Muundo wa Kiuchumi (SAPs) kulididimza zaidi uwezo wa serikali wa kuleta maendeleo. Kupunguzwa kwa upeo wa serikali chini ya sera za siasa za kupendelea mabadiliko kulisababisha kuongezeka haraka kwa mashirika yasiyo ya kibiashara ya kujitolea. Mashirika yasiyo ya kibiashara ya kibinagsi kama vile mashirika yasiyo ya kiserikali na vikundi vya kijamii vya kujitegemea, mionganoni mwa mashirika mengine, yalizuka ili kusaidia katika utoaji wa huduma za kijamii.

Licha ya ongezeko hili la idadi na shughuli za mashirika, sekta isiyo ya kibiashara bado haieleweki vyema. Imebaki imebaki katika hali ya kutotambuliwa na waundaji sera, vyombo vya habari na wasomi nchini Kenya. La kushangaza ni kwamba, hata wale weledi wa maendeleo hawana ufahamu kamili wa ukubwa na upeo wa sekta hii. Kwa jumla, hakujakuwa na uchunguzi mwafaka kuhusu uwezo wa sekta hii au hata kuhusu sifa zake za kimsingi. Zaidi ya hayo, hakuna habari nyinogi kuhusu mchango wa sekta hii katika maendeleo ya taifa. Pengo hili ndilo ambalo kwa muda mrefu limeisukuma IDS kutafiti na kutoa mchango wa habari kuhusu uwanja huu.

Kwa jumla, IDS inatoa shukrani sana kwa msaada wa kifedha uliotolewa na Aga Khan Development Network katika kusaidia kuboresha data ambayo ndiyo msingi wa kitabu hiki. Tunamshukuru Richard Hollaway (Mkurugenzi wa Civil Society, Aga Khan Development Network) na Grace Isharaza (Aga Khan Foundation-Afrika Mashariki) kwa mawaiha na juhudini zao zilizolenga kutufanikisha kazi ya kuchapisha kitabu hiki.

Mwisho, IDS ingependa kutoa shukrani maalum kwa wasomi wawili waliohusika katika kuratibu mradi huu na kutoa kitabu hiki, yaani, Dkt Karuti Kanyinga na Prof. Winnie Mitullah. Bila ya juhudini zao, ingekuwa vigumu kukamilisha mradi huu. Kwa wengine wengi waliochangia kwa njia mbalimbali, tunasema ‘asanteni sana!’

**Prof. Mohamud Jama**  
Mkurugenzi, IDS.